# Taasisi zitakazozembea kutumia e-Mrejesho kuchukuliwa hatua

**NA BILHUDA MBOWE**

**WAZIRI** wa nchi Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora George Simbachawene, amesema Serikali itachukua hatua kali kwa Viongozi wa Taasisi za Umma na watumishi watakaozembea katika matumizi sahihi ya e Mrejesho(e GA) baada ya Rais Dk Samia Suluhu Hassan kuweka mazingira mazuri na wezeshi ya Kisera na Kisheria yaliyoleta mageuzi Serikali Kidigitali.

Simbachawene ametoa kauli hiyo jana mjini Arusha wakati akifunga kikao kazi cha tano cha Serikali Mtandao, kikao kilichofanyika katika Ukumbi wa AICC.

Aliielekeza e-GA kuendelea kufanya tafiti kwa ajili ya kuleta bunifu ya mifumo ya TEHAMA itakayosaidia kuboresha Utendaji kazi na kuondoa kero za upatikanaji wa huduma mbali mbali za Serikali kwa wananchi.

Kwa Upande wake mkurugenzi mkuu wa mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA), Mhandisi Benedict Ndomba alisema katika kipindi cha siku tatu cha kikao hicho, mada mbalimbali zinazohusu Serikali Mtandao ziliwasilishwa na kujadiliwa kwa kina.

Alisema mijadala ya mada hizo, ilijikita kwenye umuhimu wa ubunifu katika utekelezaji wa jitihada za serikali mtandao, kwa ajili ya kuboresha utendaji kazi katika taasisi za umma na utoaji wa huduma kwa Umma.

"Mada hizo ziliwasilishwa na wataalamu wa TEHAMA, kutoka katika taasisi mbalimmbali za umma na binafsi na kisha washiriki walipata nafasi ya kujadiliana juu ya mada hizo na kubainisha namna bora ya kutekeleza jitihada za Serikali Mtandao, kuainisha changamoto zilizopo na namna bora ya kukabiliana na changamoto hizo."alisema na kuongeza

"Kupitia majadiliano hayo, washiriki wameweka maazimio, ambayo sisi Mamlaka tunaahidi kuyafanyia kazi, ili kuhakikisha yanatekelezwa kwa wakati, lakini pia tupo tayari kupokea maelekezo yako utakayoyatoa hapa leo kwa ajili ya utekelezaji.

Aliongeza kuwa mamlaka inaahidi kuendeleza ushirikiano mzuri uliopo miongoni mwa taasisi za Umma na binafsi, ambao ni wadau muhimu wa serikali mtandao, ili kwa pamoja waweze kutatua changamoto mbalimbali zilizopo katika jamii kupitia TEHAMA.

"Nikuhakikishie wewe Mhe.Waziri pamoja na washiriki wote waliopo hapa kuwa, Mamlaka itaendelea kushirikiana na Taasisi za Umma katika Kubuni, Kusanifu na Kujenga Mifumo mbalimbali ya TEHAMA, itakayosaidia kutatua changamoto zilizopo katika jamii yetu, itakayowezesha Serikali kutoa huduma kwa wananchi kwa urahisi, haraka na kwa gharama nafuu zaidi. "

Alisema pamoja na mikakati mbalimbali ambayo wamejiwekea kama Mamlaka, kwa lengo la kuhakikisha Serikali Mtandao inaimarika, pia aliiomba Serikali kupitia Wizara ya Utawala Bora kuendelea kuweka mazingira wezeshi kwa Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA), ili iweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi na weledi wa hali ya juu, katika kuhakikisha Serikali ya kidijitali inafanikiwa zaidi.

**Makonda ashukuru**

Akizungumzaa katika kikao hicho Mkuu wa mkoa wa Arusha, Paul Makonda alisema kipekee kabisa wanapenda kuishukuru na kuipongeza Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA) kwa kuandaa Kikao Kazi hicho, ikiwa ni hatua ya kuipeleka mbele Serikali Kidijitali.



*Waziri wa nchi Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora George Simbachawene*

Alisema Wakazi wa Mkoa wa Arusha wamefarijika na kufurahi kupata ugeni huo, hususani kuona e-GA ikiendelea kuliamini na kulichagua jiji letu la Arusha, kuwa mwenyeji wa vikao kazi hivyo kwa mara ya tano (5) sasa.

Kwa Upande wake Katibu Mkuu Ofisi ya Rais Ikulu, Mululi Mahendeka alieleza kuwa Kikao Kazi hicho cha siku tatu cha Serikali Mtandao, kimewakutanisha wadau zaidi ya 1,000 wa Serikali Mtandao kutoka katika Wizara, Mashirika na Taasisi za Umma, ili kujadiliana na kujenga uelewa wa pamoja kuhusu utekelezaji wa jitihada za Serikali Mtandao.

Alisema Vikao hivyo vimekuwa na manufaa makubwa katika kukuza na kuendeleza jitihada za Serikali Mtandao, kupitia mawazo mbalimbali yanayotolewa na washiriki wa vikao.

Alimuhakikishia Waziri Simbachawene kuwa wao watasimamia utekelezaji wa maazimio yote yaliyofikiwa kwenye kikao hicho kwa wakati, ikiwa ni kwa Wizara yenyewe, e-GA au taasisi nyingine ya umma inayohusika.

"Kama tulivyofanya mwaka huu, taarifa ya utekelezaji wa maazimio haya yatawasilishwa katika Kikao Kazi kijacho."alisema Mahendeka.

Mwenyekiti wa bodi ya wakurugenzi ya e-Ga Dk Musa Kissaka, alitumia mkutano huo kuwashukuru waandishi wa Habari kwa ushiriki wao na kwa mchango mkubwa wanaoutoa katika kutangaza kazi mbalimbali za Mamlaka.

"Ninyi ni wadau muhimu na tunathamini mchango wenu, katika kuhamasisha matumizi ya Serikali Mtandao kupitia kalamu zenu."alisema

# Ulega: Ubunifu wa kuondoa foleni utaongeza mapato ya Serikali

**NA MWANDISHI WETU**

**WAZIRI** wa Ujenzi, Abdallah Ulega, amewataka wataalamu wa wizara hiyo kutumia Mkutano wa Baraza la Wafanyakazi uliofanyika mkoani Singida kubuni njia zitakapunguza foleni mijini na kuongeza mapato ya serikali.

Akizungumza wakati wa uzinduzi wa mkutano wa Baraza hilo, Waziri Ulega alisema pamoja na mkutano huo kuwa na ajenda zake za kawaida kisheria, ni muhimu masuala muhimu kama ya foleni ambayo yanagusa wananchi wengi yakajadiliwa kwa kina kwa sababu mkutano huo umesheheni wataalamu wa kutosha.

]Akizungumza kwa mifano, Ulega alisema binafsi anaona fursa ya kupunguza kero ya foleni na serikali kujiongezea mapato endapo ubunifu utafanywa kwenye maeneo ambako kuna barabara za mwendokasi.

"Hivi hakuna namna ambayo kwa kulipia, magari ya kawaida yanaweza kutumia njia ya Mabasi Yaendayo Haraka (BRT) endapo njia za kawaida zitakuwa na foleni? Kwa nini barabara moja ikae nusu saa bila gari kupita wakati kwingine hakuendeki kwa sababu ya foleni?

"Kwenye daraja la Mwalimu Nyerere tunafanya hivyo tayari kwa PPP na watu wanalipa kuvuka daraja. Nchi nyingine watu wanalipia kutumia baadhi ya barabara kama hawataki foleni. Naamini tunaweza kufanya kitu lakini tunahitaji wataalamu mtushauri," alisema Ulega.

Katika hatua nyingine, Ulega amewaagiza watumishi wa Wizara ya Ujenzi kuhakikisha wanazingatia thamani ya fedha wakati wa utekelezaji na usimamizi wa miradi mbalimbali nchini ikiwemo barabara, madaraja, vivuko, majengo ya Serikali na viwanja vya ndege.

"Nawaelekeza muendelee kuunga mkono dhamira hii njema ya Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuhakikisha thamani ya fedha inaonekana kwenye miradi mnayoisimamia", amesema Ulega

Aidha, Ulega ameuagiza Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS) kuongeza juhudi za usimamizi wa utekelezaji wa miradi ya dharura ya miundombinu ya barabara iliyoharibiwa na mvua El-Nino na Kimbunga Hidaya yenye thamani ya Shilingi takriban bilioni 868.56.

Ameelekeza Viongozi wa Wizara kwa kushirikiana na Baraza la Taifa la Ujenzi (NCC), kuhakikisha kuwa dhana ya uwezeshaji wa Makandarasi wa ndani inatekelezwa kama ilivyokusudiwa ili kunufaisha na kuwajengea uwezo makandarasi wazalendo.

Kwa upande wake, Mkuu wa Mkoa wa Singida, Halima Dendego ameipongeza Wizara ya Ujenzi kwa kuendelea kuufungua mkoa wa Singida kwa ujenzi wa miundombinu ya barabara za lami ambazo zimesaidia kurahisisha huduma za usafiri na usafirishaji katika mkoa huo.

Naye, Mwenyekiti wa Baraza hilo na Katibu Mkuu wa Wizara ya Ujenzi, Balozi, Mhandisi, Aisha Amour amesema kuwa Wizara inaendelea kutekeleza miradi mbalimbali ya kimkakati ikwemo ujenzi wa Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Msalato, ujenzi wa daraja la Kigongo- Busisi na ujenzi wa daraja la Mwendokasi (BRT) jijini Dar es Salaam.

Mkutano wa Baraza la Wafanyakazi la Sekta ya Ujenzi umefanyika mkoani Singida ambapo ajenda kuu katika Mkutano huo ni kupokea, kujadili na kuidhinisha Bajeti ya Wizara ya Ujenzi kwa mwakawa fedha 2025/26 kabla ya Bajeti hiyo kuwasilishwa kwenye Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kushirikisha wajumbe mbalimbali kutoka Wizarani na Taasisi zilizo chini ya Wizara.



*Waziri wa Ujenzi, Abdallah Ulega*